**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Thelathini na Mbili – Tarehe 15 Juni, 2026**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua Zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti:**

Hotuba ya maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Mpango wa Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2026/2027.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

228. MHESHIMIWA MAKAME MOHAMED SUFIANI (Jimbo la Chumbuni)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Je, ni upi mpango wa Serikali katika kuzijenga Ofisi za masheha katika maeneo ambayo hazijajengwa.

**Wizara ya Fedha na Mipango:**

416. MHESHIMIWA JUMA HASSAN THABIT (Jimbo la Fuoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Moja ya jukumu la Mamlaka ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma, ni kusimamia Kada ya Ununuzi pamoja na kutoa miongozo

mbalimbali ya kimanunuzi. Kwa vile sasa manunuzi yote hufanyika kwa kutumia mifumo.

Je, Mamlaka iimetoa mapendekezo yoyote katika kuboresha Mitaala ya Vyuo vya Kati na Vyuo Vikuu (Procurement with IT), vitakavyoweza kuwasaidia wafanyakazi wa Kitengo cha Ununuzi kuwa na uwezo wa matumizi ya mifumo ya *E-Proz System.*

**<u>Wizara ya Kazi na Uwekezaji:</u>**

150. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Uwekezaji:

Katika jitihada za kuvutia uwekezaji nchini, Serikali inatoa vivutio mbali mbali kwa uwekezaji, ikiwemo misamaha ya kodi na upatikanaji wa ardhi;

Je, ni kwa kiasi gani uwekezaji huo unaleta manufaa ya moja kwa moja ukilinganisha na vivutio vikubwa vinavyotolewa kwa wawekezaji.

**<u>Wizara ya Afya:</u>**

286. MHESHIMIWA ALLEY MASOUD ALLEY (Jimbo la Mtambile) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Pamoja na Kituo cha Afya cha Mtambile kujengwa na kutarajiwa kutoa huduma za msaa 24, ujenzi huo haukujumuisha nyumba hata moja ya madaktari na wahudumu wengine wa afya;

Je, Wizara ina mpango gani wa kujenga Nyumba za Madaktari katika kituo hicho.

290. MHESHIMIWA ALLEY MASOUD ALLEY (Jimbo la Mtambile) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kutokana na hali ya Kituo cha Afya cha Kisiwa Panza kuwa chakavu na kutokidhi sifa za kuwa Kituo cha Afya.

Je, ni lini Serikali itakijenga upya kituo hicho na kuboresha huduma zote muhimu zinazopaswa kuwepo katika Vituo vya Afya.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

344. MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (Jimbo la Ole) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Hivi karibuni kumezuka tabia ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kutembea na Askari wa Idara Maalum, kukamata na kupiga wananchi ambao wamekamatwa na gari za mchanga.

(a) Je, ni ipi kauli ya Serikali kuhusiana na tabia hii.

(b) Je, kwa kiasi gani vitendo hivyo vinaifanya Serikali ionekane inafanya makosa ya jinai kwa kuwapiga na kuwaumiza wananchi bila ya kufuata taratibu za kuwapeleka katika vyombo vya sheria.

425. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kumekuwa na upungufu mkubwa wa ukosefu wa maji katika jimbo la Micheweni na maeneo mengine.

Je, kuna utaratibu gani wa ziada wa kuliondoa tatizo hilo.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

240. MHESHIMIWA ABDULGHANI ISMAIL ZUBEIR (Jimbo la Malindi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Pongezi za dhati kwa Serikali ya Awamu ya Nane kwa kuchukua hatua madhubuti za kukarabati majengo ya Mji Mkongwe ikiwemo majengo ya Shirika la Nyumba la Zanzibar (ZHC). Hata hivyo, baada ya ukarabati wa majengo hayo, ZHC imepandisha kodi kwa nyumba hizo ikizingatia thamani na tathmini husika ya ukarabati.

(a) Je, ZHC imefanya tathmini gani ya kodi mpya inazoziweka kulinganisha na zile kodi zilizokuwepo awali ili kuendana na kipato husika cha wakaazi wa nyumba hizo.

(b) Je, ZHC imeweka utaratibu gani madhubuti wa kuwahakikishia wakaazi waliokuwemo awali kabla ya ukarabati ndio hao watakaorejeshwa kuendelea kuzitumia nyumba hizo baada ya ukarabati.

(c) Kwa kuwa wananchi wengi wanaotumia nyumba hizo ni wa kipato cha chini na baadhi hushindwa kumudu kodi mpya, je Serikali ina mpango gani wa kutoa ruzuku *ya* kodi za nyumba

hizo *(subsidize)* kwa Mji Mkongwe tu kama inavyofanyika katika sekta zengine ikiwemo mafuta na kilimo kwa lengo la kuhifadhi tamaduni za Mji Mkongwe ulio chini ya hifadhi ya UNESCO.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaj, Maliasili na Mifugo:**

334. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Machinjio ya wanyama ni miundombinu muhimu katika kuhakikisha ubora na usalama wa nyama kwa matumizi ya binadamu.

Je, Serikali imejipangaje kuboresha na kusimamia ubora wa machinjio yaliyopo katika Jimbo la Chake Chake, ili kulinda afya ya wananchi.

**Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:**

153. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Je, Serikali imejipanga vipi katika kuimarisha barabara hatarishi kwenye maeneo yanayoripotiwa kuwa na ajali nyingi.

469. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi

Tarehe 12/4/2026 Kitengo cha Ukaguzi wa Magari Kaskazini Pemba Wete, saa 11 za alfajiri, kilikamata gari ikiwa safarini kupeleka mgonjwa hospitali. Ni jambo la kushangaza kuona saa 11 alfajiri, Kitengo hicho kinafanya kazi na kuzuwia gari hiyo ambayo inawasaidia wananchi wa jimbo la Ole katika huduma za usafiri za kwenda hospitali. Aidha, cha kushangaza zaidi ni kitendo cha kutolewa ‘Plate Number’ ya gari hiyo na kutozwa Tsh. 600,000/- ikapunguzwa mpaka Tshs 349,500/- huku msimamizi wa gari hiyo akiiacha mpaka leo hii.

(a) Je, kuna sheria iiliyoletwa hapa Barazani ya kutoa faini kama hii na kuzifungua ‘Plate Number’.

(b) Je, wanaosimamia kazi hii wako tayari kupelekwa kwenye chombo kinachofuata sheria za nchi hii.

(c) Kutokana na jiografia ya Pemba, na baada ya kuizuia gari wanayotoa huduma kwa nananchi, je Wizara imechukua hatua gani kwa watendaji hao.

**<u>Wizara ya Biashara na Maendelo ya Viwanda:</u>**

202. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Asili ya Zanzibar ni kuwa Kitovu cha Biashara tangu karne nyingi zilizopita. Hali hii iliwapelekea watu wengi kuja Zanzibar kibiashara na kuifanya Zanzibar na watu wake kunufaika kiuchumi kwa kiasi kikubwa.

(a) Kwa sababu gani Serikali haioni haja ya kuanzisha Bandari Huru kwa bidhaa zinazoingia ndani ya Zanzibar na kutoza ushuru kwa bidhaa zinazotoka kwenda kwenye Masoko ya Kikanda na Kimataifa.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kukuza masoko ya bidhaa zote ndani ya Zanzibar, ili kuchochea kukua biashara Zanzibar.

**<u>Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:</u>**

208. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:

Ubunifu wa sayansi ya teknolojia ni jambo linalokuwa kwa kasi na maendeleo ya nchi yoyote duniani, ili kuweza kudhibiti mifumo hiyo, kunahitajika uwekezaji mkubwa wa kulinda Mifumo ya Mawasiliano.

(a) Ni upi mpango wa Serikali katika kuzuia uhalifu wa mitandaoni kwa wananchi wa Zanzibar.

(b) Ni tathmini ya maafisa wangapi waliotambuliwa na Serikali katika fani ya Udukuzi wa Mitandao (Hackers).

(c) Ni matukio mangapi yaliyoripotiwa kwa Zanzibar juu ya Udukuzi wa Mitandao.

**<u>Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:</u>**

176. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Dhana ya utalii kwa wote na kuwezesha utalii wa ndani kwa wananchi wa Zanzibar, imekuwa haitekelezwi vya kutosha hapa nchini na Serikali haijaweka mkazo madhubuti katika kuhamasisha kuongeza watalii wa ndani. Hata hivyo, kwa siku za hivi karibuni, kumeibuka aina mpya ya Utalii wa Mikutano (Conference Tourism) ambao huweza kukusanya *delegates* kutoka mataifa mbalimbali jambo linaloiwezesha nchi kuongeza idadi ya watalii.

(a) Je, Serikali ina mpango upi wa kujenga Kituo cha Kimataifa cha Mikutano (International Conference hall) hapa Zanzibar.

(b) Ni upi mpango wa Serikali wa kuanzisha programu maalum za kuutangaza utalii wa ndani kwa jamii ya Kizanzibari.

(c) Kwa kuwa tozo zinazowekwa kwenye utalii wa ndani (Domestic Tourisrm) ni kama zinafanana na zinazotozwa kwa wageni kutoka nje, je, ni ipi kauli ya Serikali kwa sehemu hizi za vivutio vya utalii.

**<u>Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji:</u>**

309. MHESHIMIWA MAHFOUDH ABDALLA MOHAMMED (Jimbo Magomeni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Vijana, Ajira na Uwezeshaji:

Kumekuwa na programu nyingi za uwezeshaji wananchi kiuchumi, hasa wanawake katika Serikali hii ya Awamu ya Nane.

(a) Je, ni vikundi vingapi kati ya vikundi 55 vya kinamama vyenye usajili, vilivyopo katika jimbo la Magomeni, vimeshafaidika na programu hizo za uwezeshaji hasa mikopo.

(b) Kwa wale ambao bado hawajafikiwa na neema hizo licha ya shauku kubwa waliyokuwa nayo ya kujikomboa kiuchumi, je Serikali inawashauri wafanye nini ili na wao wafaidike na matunda na nia njema ya Rais wao ya kuwakomboa wananchi wake.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

137. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Je, Wizara ina mikakati gani ya kulinda mazingira ya bahari na fukwe ili kuhakikisha rasilimali za bahari zinaendelea kudumu kwa vizazi vijavyo.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Fedha na Mipango:**

Kwamba Baraza hili lijadili na Kuukubali Mpango wa Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2026/2027 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2026/2027.

**Zanzibar,**
**15 Juni, 2026.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA LA WAWAKILISHI, ZANZIBAR.**